MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA


**Na: 17. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Machi 11-20, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Machi 21-31, 2018**

**Muhtasari**

- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wanaendelea na shughuli za upandaji na palizi.
- Hali ya unyevunyevu uliokithiri katika udongo na maji yaliyosimama mashambani vinaweza kuathiri maendeleo ya mazao hususan shambani yaliyoko mabondeni.
- Wakulima, wavuvi, na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa hii.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2018

Katika kipindi hicho, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo. Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kubaki katika maeneo ya Tanzania. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani na kusababisha upepo kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine kumekuwepo na joto la bahari la chini kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).




**Kielelezo**. Kiasi cha mvua (%) kipindi cha tarehe 11-20, Machi 2018.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, maeneo mengi ya nchi pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua za juu ya wastani (zaidi ya 124% ya wastani wa mvua kwa siku kumi). Hata hivyo, mvua za chini ya wastani (chini ya 75% ya wastani wa mvua kwa siku kumi) zilinyesha katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Songwe, Njombe, Kigoma na Ruvuma kama inavyoonekana kwenye kielelezo.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, mvua zilizonyesha zilitoa mwelekeo mzuri wa hali ya mazao pamoja na malisho ya mifugo, licha ya maeneo machache kupata unyevunyevu uliokithiri katika udongo na maeneo mengine kuwa na hali ya ukavu. Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, mahindi yalikuwa katika hatua ya kutoa ya kubebe na mengine yakikaribia kukomaa haswa mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Dodoma, Singida, Tabora Kigoma, Ruvuma na Mtwara. Wakulima katika maeneo hayo walijishughulisha zaidi na palizi pamoja na upandaji ya mazao kama vile maharage na viazi vitamu. Wakulima katika maeneo

yanayopata misimu miwili ya mvua waliendelea kupanda na palizi. Hata hivyo, mahindi yaliyochelewa kupandwa msimu wa vuli yameripotiwa kuvunwa mikoa ya Simiyu na Shinyanga. Upande wa malisho na upatikanaji wa maji, hali imeendelea kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan katika mabonde ya Rukwa, Nyasa na Rufiji kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2018

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika kidogo wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo. Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kubaki katika maeneo ya Tanzania. Joto la bahari katika maeneo ya kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani na kusababisha upepo kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine kumekuwepo na joto la bahari la chini kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola)

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2018

**Kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara),** na **kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro)** na **nyanda za juu Kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa)** yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

**Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)** na **nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro)** yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora)** na **pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi)** panatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache. **Katikati mwa nchi** (**mikoa ya Dodoma na Singida**) panatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31,2018

Hali ya mvua zinazotarajiwa zitasaidia kuboresha ukuaji na maendeleo ya mazao pamoja na malisho. Hata hivyo, unyevunyevu uliokithiri katika udongo pamoja na mvua nyingi vinaweza kuathiri shughuli za palizi na uwekaji mbolea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua. Kutokana na mvua zinazotarajiwa, maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hali ya unyevunyevu kwenye udongo inatatarajiwa kuimarika na kusaidia ukuaji wa mazao. Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo vinatarajiwa kuimarika kwenye maeneo mengi ya nchi. Wakulima, wavuvi, na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31,2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua zinazotarajiwa. Wananchi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uvunaji maji ya mvua na kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***